

Chanjo za UVIKO -19 hapa Nova Scotia

Umri wa miaka 12 na zaidi



Umri wa miaka 12-17

Mfululizo wa Msingi - Pfizer (asili)

Dozi ya nyongeza - Pfizer Bivalent

Umri wa miaka 18 na zaidi

Mfululizo wa Msingi

Pfizer au Moderna (asili)

Dozi ya nyongeza

Pfizer au Moderna Bivalent

Vipindi vilivyopendekezwa kati ya dozi

Kati ya dozi za mfululizo za msingi

Dozi 1 hadi 2 - **Wiki 8** (siku 56)

Kati ya mfululizo wa msingi na nyongeza, au kati ya dozi za nyongeza

Miezi 6 (siku 168)

Wanovia Scotia ambao wana **kinga daifu kiasi au sana** watahitaji dozi ya tatu ya chanjo ili kukamilisha safu yao ya msingi.

- ✓ Dozi 1 hadi 2 - **Wiki 4** (siku 28)
- ✓ Dozi 2 hadi 3 - **Wiki 8** (siku 56)

Chanjo Baada ya Kupona UVIKO -19

Baada ya kupona UVIKO-19, unapaswa kusubiri **wiki 8** ili kupata mfululizo wako wa msingi. Ikiwa umekamilisha mfululizo wako wa msingi, unapaswa kusubiri kwa **miezi 6** ili kupata dozi yako inayofuata ya nyongeza.



Chanjo zote za mRNA (Pfizer na Moderna) ni **salama, zenye ufanisi na zinapendekezwa sana** kwa chanjo ya UVIKO-19. Kwa baadhi ya makundi ya umri, mwongozo wa ziada juu ya uchaguzi wa chanjo hutolewa:

- » Watu wenye umri wa miaka 12-29 wanashauriwa kupata Pfizer (asili) kwa safu yao ya msingi.
- » Watu wenye umri wa miaka 12-29 ambao wana kinga dhaifu kiasi au sana wanaweza kuchagua kupata Moderna (asili) kama mbadala.
- » Watu wenye umri wa miaka 18 na zaidi wanaweza kuchagua chanjo mbadala ikiwa hawawezi au wangependelea kutopata chanjo ya mRNA. Tembelea www.nshealth.ca/coronavirusvaccine kwa maelezo zaidi (kwa Kiingereza pekee).

Chanjo za bivalent

Afya ya umma inapendekeza kwamba Wanovia Scotia **wenye umri wa miaka 5 na zaidi** ambao wamekamilisha safu yao ya msingi wapate chanjo ya bivalent badala ya chanjo ya awali ya mRNA kwa dozi yao inayofuata. Pamoja na kwamba chanjo zote zinatoa ulinzi mzuri, bivalent ina uwezekano mkubwa wa kukinga dhidi ya lahaja ya Omicron ya UVIKO -19.

“Bivalent” inamaanisha kuwa chanjo inalinda dhidi ya aina mbili tofauti (aina ya asili/lahaja) za virusi vya UVIKO-19: aina ya asili na aina ya Omicron. Chanjo hizi za bivalent husaidia kujenga mwitikio mpana wa kinga na kuboresha nguvu na muda wa ulinzi.